**HOTUBA YA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA JENGO LA UWEKEZAJI LA ZSTC (KARAFUU HOUSE), MADUNGU CHAKE CHAKE, PEMBA TAREHE 09 JANUARI, 2024**

**Mapinduzi! Mapinduzi! Mapinduzi!**

*Mheshimiwa Omar Said Shaabani, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar,*

*Mheshimiwa Mattar Zahor Masoud, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba*

*Mheshimiwa Salama Mbarouk Khatib, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba,*

*Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Chake na Mkoani Pemba,*

*Wakuu wa Vikosi vya ulinzi na usalama mliohudhuria,*

*Ndugu Ali Khamis Juma, Katibu Mkuu, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar,*

*Ndugu Soud Said Ali, Mkurugenzi Mwendeshaji, Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar,*

***Viongozi wa Chama Tawala (CCM) na Viongozi wa vyama Vingine,***

***Viongozi wa Taasisi za Umma na Taasisi binafsi,***

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

***Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.***

**Assalamu Alaykum,**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**SALAAM**

Kwanza ni shukrani kwa Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kukutana leo katika kazi hii ya kufungua jengo hili. Mara ya mwisho nilivyokuja hapa nilikuta mabati, na sikujua ndani ya mabati kuna nini. Kumbe yale mabati yakifunguliwa kuna neema kubwa sana ndani. ***Mabati Oyeee!***

Aidha, nitumie fursa hii pia kuishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa jengo hili la uwekezaji la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar – ZSTC, maarufu kama ***Karafuu Investment House***, ikiwa ni sehemu ya Sherehe ya kutimiza Miaka 60 ya Mapinduzi

Matukufu ya Zanzibar. Hivyo, asanteni sana, sana kwa kunipa fursa hii kuja Pemba kufanya ufunguzi wa jengo hili.

Waswahili wanasema shughuli ni watu, na watu hapa tumetimia. Tumetimia haswa. Niwashukuruni wote mliokuja hapa, na mliokuja kunisalimu dada yenu. Asanteni sana.

**UZINDUZI WA JENGO LA KARAFUU**

**Ndugu Wananchi,**

Kwa dhati kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda na uongozi wa ZSTC kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuliendeleza zao la karafuu hapa kwetu Zanzibar. Leo tunakutana kwa sababu ya kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na shirika hili, ujenzi wa jengo la kisasa hapa Pemba. Niwapongeze pia Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa mradi huu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Wote kwa ujumla Hongereni sana!

Uwepo wa jengo hili ni kielelezo cha ustawi wa zao letu la karafuu. Pia ni ushahidi tosha wa kazi nzuri inayofanywa na wakulima wetu wa karafuu. Kwa upande mwingine niwapongeze

sana na kuwashukuru wakulima wa zao la karafuu, kwa sababu bila ari na jitihada zao tusingepata mawazo ya kusema tujenge jengo kama hili. Bila shaka kazi yao kubwa na nzuri ndio imetufanya tuwaze kujenga jengo hili.

Sio tu kujenga jengo hili, pia wana mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo. Tunapopima maendeleo ya uchumi, sekta ya kilimo tunaiona iko juu. Hii ni kwa sababu ya zao la karafuu. Wanafanya jitihada za kukuza uchumi wa nchi yetu kwa ujumla. Kwa hiyo niwapongeze sana kuwashukuru wakulima wa karafuu hapa Zanzibar, Pemba na Unguja.

Ufunguzi wa jengo hili ni hatua moja mbele, kwani, jengo hili litawarahisishia wakulima kuuza karafuu zao, ndio maana likajengwa katika kisiwa cha Pemba, kwa sababu karafuu nyingi sana inatoka Pemba. Karafuu zinazouzwa zitahifadhiwa kwenye maghala safi na ya kisasa. Ndugu zangu, nilipofika tu hapa, nilikwenda kutembezwa kwenye hili jengo, maeneo ambako karafuu inanuliwa na maeneo ambako karafuu itahifadhiwa. Ni maeneo mazuri. Kilichonifurahisha zaidi ndugu zangu ni kwamba

sasa karafuu inanuliwa kisayansi. Ile enzi ya kununua karafuu kwa mkono, na kumwambia mkulima karafuu yako ina unyevu mkubwa, *grade* (daraja) yake ya pili, sasa haipo. Haipo dhulma ile, haipo. Kwa sasa kila kitu ni mashine. Unyevu unapimwa kwa mashine, *grade* (daraja) itapatikana kutokana na unyevu uliooneshwa kwenye mashine. Hata kuisafisha, inakwenda kusafishwa kwa mashine. Sasa karafuu inayotoka Zanzibar kwenda nje ni safi na yenye viwango vya hali ya juu kiasi ambacho tunakwenda kulitawala soko la karafuu nje. Hii ni hatua kubwa, na ninawashukuru sana.

Katika jengo hili pia kuna huduma za kibenki zitakazomrahisishia mkulima au muuzaji wa karafuu huduma za kifedha. Ataamaua kama fedha yake iingizwe benki, atiliwe kwenye simu au apewe mkononi pesa yake, ataamua yeye mwenyewe. Vilevile kuna maduka ambayo wananchi wa eneo hili wanaweza kunufaika kama wapangaji au kufanya biashara zao ndani ya eneo hili.

Niseme tu nimefarijika kuwa sehemu ya historia ya jitihada hizo za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia uzinduzi wa jengo

hili la kisasa. Rai yangu kwa ZSTC, ni kuhakikisha kuwa jengo hili linatumika ipasavyo ili lifikie malengo yake katika kuendeleza zao hili. Imesemwa hapa kuwa jengo hili ni kitega uchumi, kwa hiyo matumaini yangu ni kwamba Shirika watalitumia jengo hili vyema kutafuta fedha, hali ambayo haitalazimisha Hazina ya Serikali kutoa fedha kuwapatia shirika. Jengo hili litatoa fedha zaidi kwa shirika kwa sababu litafanyiwa biashara.

**UMAALUM WA ZAO LA KARAFUU**

**Ndugu Wananchi**,

Zao la karafuu limeendelea kuwa muhimu kwa uchumi na maendeleo yetu Zanzibar. Karafuu ni moja kati ya zao kongwe sana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba lililoanza tangu karne ya 19. Karafuu imekuwa ikitamba tangu karne ya 19 huko, kwa hiyo tunaweza kusema, *karafuu ni almasi yetu Zanzibar!* hatuna budi kuitunza, kuienzi na kuiendeleza.

Tangu Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar zao hili limeendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar. Hadi sasa zao hili linashikilia namba moja kwenye mauzo ya Zanzibar nje ya nchi. Tunapoelekea kwenye uchumi wa bluu, tutapata mazao ya

uchumi wa bluu yashike namba mbili, lakini karafuu inaendelea kushika namba moja.

Kwa mfano, mwaka 2022 mauzo ya karafuu nje ya nchi yalichangia shilingi za kitanzania **bilioni 118** sawa asilimia **65.6** ya mauzo yote ya Zanzibar. Hii ni sehemu kubwa kwa zao hili.

Kupitia zao hili, visiwa vya Unguja na Pemba, *vimejipatia jina maarufu la visiwa vya marashi ya karafuu au visiwa vya viungo.* Kimataifa, Zanzibar imeendela kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa karafuu na karafuu inayotoka Zanzibar ina hadhi na ladha ya kipekee sana. Huko nyuma tulikuwa hatujui, tunauza karafuu zetu kwa mtu moja au watu wawili wanaichukua na kwenda kuichanganya na ya Brazil na Indonesia. Wanaiongezea hadhi karafuu yao halafu wanakwenda kwenye soko kubwa kuiuza ikiwa na karafuu yetu imechanganywa humo. Lakini leo tunakwenda wenyewe kwenye soko, na karafuu yetu inakwenda yenyewe kwenye soko. Ndio maana bei nayo inakuwa sio haba, *Alhamdullilah,* haianguki sana.

Kwa kuzingatia upekee wa umaarufu wa karafuu yetu Zanzibar katika soko la kimataifa, sote kwa hiyo hatuna budi

kuhakikisha kuwa umaarufu huo, au chapa (brand) ya karafuu ya Zanzibar inabaki na inalindwa kwa kuzingatia viwango vya karafuu inayouzwa nje ya nchi. Kwa yale ambayo nimeoneshwa kule ambapo karafuu inanunuliwa, sina shaka ile *brand (*sifa*)* yetu tutaendelea kuitunza.

**SERIKALI KUTOA KIPAUMBELE KWA KARAFUU**

**Ndugu Wananchi**,

Serikali za awamu zote tangu Mapinduzi zimelipa zao hili kipaumbele stahiki. Ninakumbuka kati ya mwaka 2005 na 2010 nilipokuwa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tulilipa zao la karafuu kipaumbele licha ya changamoto ya kibajeti kwa wakati ule, hali iliyoilazimu hadi kuchukua mikopo Benki ya Watu wa Zanzibar ili kununua karafuu kutoka kwa wakulima. Wakati ule fedha zilikuwa sio nyingi, tulikuwa tunakopa, tunanunua karafuu, tukiuza tunalipa mikopo, na faida tunayopata tunaendeleza zao.

Changamoto nyingine tulizokutana nazo ni baadhi ya wakulima kuvuna karafuu kwa kuchelewa, kiasi ambapo tunapokwenda kwenye soko la dunia, pamoja na uzuri wa karafuu

yetu, karafuu inakuwa imeshuka bei kwa sababu wengine wamevuna.

Changamoto nyingine ilikuwa ni magendo ya karafuu. Tulipambana sana na jambo hili. Kule ndani niliulizia suala hili na nikaambiwa bado lipo. Sasa ndugu zangu niseme, karafuu ndio maendeleo yetu. Asilimia 65.6 ya mauzo yetu nje yanatokana na karafuu. Tunapoichepusha na kuiuza nje tunafifisha maendeleo yetu wenyewe. Tunapotaka barabara zijengwe pesa zitatokana na mauzo ya karafuu. Mnapoichepusha na kuiuza nje tunafifisha maendeleo yetu wenyewe, wala hatuikomoi Serikali, tunajikomoa wenyewe wananchi. Karafuu ndio dhahabu yetu, ndio almasi yetu Zanzibar. Acheni Serikali ifanyie kazi, tulete wawekezaji zaidi waongeze mnyonyoro wa thamani kwenye karafuu. Tuuze mauzo ambayo sio karafuu ghafi, bali tuuze mazao yanayotokana na karafuu ili tupate faida zaidi.

Pamoja na hayo wakati ule tuliendelea kuhakikisha kuwa ZSTC inafanikiwa kununua karafuu kutoka kwa wakulima na tuliendelea kusisitiza umuhimu wa kuliendeleza zao hili.

Vilevile, ili kuimarisha Shirika letu hili, nakumbuka tulimleta Mshauri Elekezi, kufanya utafiti kuhusu Muundo wa ZSTC, na nakumbuka utafiti huo ulichangia maboresho ya Sheria ya ZSTC (Na. 11 ya 2011), Sheria inayotumika hadi sasa, na mi nafurahi kuwa ndani ya historia hiyo. *Asanteni sana.*

**Ndugu wananchi**

Mtamkumbuka miaka 1960 hadi 1978 zao hili lilizalishwa kwa kiwango kikubwa sana kilichofika hadi **tani 20,000** kwa mwaka. Kutokana na changamoto mbalimbali zilizotukumba wakati ule, uzalishaji ulishuka hadi wastani wa tani **8,000** kwa mwaka 2020. Hivyo, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 ni kuongeza uzalishaji wa karafuu hadi kufikia **tani 10,000**. Hayo ndio maelekezo ya Ilani, na nina uhakika kuna hatua zinachukuliwa ili kufikia malengo hayo. Nimefarijika na mkakati unaowekwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Nilipoulizia kuhusu mavuno ya msimu huu, niliambiwa wanategemea kununua kama tani 5,000 kwa msimu huu. Tuna misimu miwili ya kutupeleka hadi tani 10,000 kwa mwaka kama ilivyoelezwa na Ilani.

Ninafarijika pia kuona jitihada za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuelekea tena kwenye tani 20,000 kwa mwaka. Nami niwatie moyo, na niseme kwamba mtakapohitaji ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tupo tayari kusaidia.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeendelea kuimarisha bei ya karafuu ili kuendana na soko la kimataifa. Kwa msimu ulioanza mwezi Agosti 2023, bei kwa kilo ya karafuu ya daraja la kwanza ilipanda kutoka **Shilingi 14,000** hadi **Shilingi 15,000.** Nilipoondoka mimi bei ya karafuu ilipanda kutoka 3,500 hadi 8,500. Kufika 15,000 ni hatua kubwa sana. Hongereni sana. Kupitia ongezeko hilo la bei inakisiwa kiasi cha shilingi **Bilioni 76.46** zinakwenda kwa wakulima; wakulima watafaidi fedha hizo. Serikali pia imeweka mikakati ya kuimarisha mnyonyoro mzima. Tunakwenda kuongeza thamani ya zao la karafuu, kutengeneza mazao yatokanayo na karafuu na sio kuuza karafuu yenyewe ikiwa ghafi. Tutafuta wawekezaji na kuwaelekeza kuja Pemba ili kuongeza thamani ya karafuu.

Dhamira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwenye kuendeleza zao hili, iko wazi. Hivyo, wakulima wa zao la karafuu tunayo kila sababu ya kutembea kifua mbele, kwa kuwa Serikali inatuthamini na inatoa umuhimu wa kipekee kwa sekta ya kilimo, hususan zao karafuu. Kwa hiyo, hatuna budi kuendelea kuzalisha kwa wingi zaidi ili tuendelee kuchochea ustawi na maendeleo kwa ujumla.

## MABORESHO KWENYE UZALISHAJI WA KARAFUU

**Ndugu Zangu,**

Niseme tu kwamba, mahitaji ya soko la kimataifa bado ni makubwa. Bado soko lipo. Kila tunapozalisha bado hatujaweza kukidhi mahitaji ya soko. Kwa hiyo bado tuongeze jitihada kwenye uzalishaji. Kwa muktadha huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Balozi zake na kupitia majukwaa mbalimbali itaendelea na jitihada za kuendelea kufungulia masoko karafuu yetu. Tulivyokuwa India tumepata soko la karafuu, na tutaendelea kufanya hivyo.

Lakini wakati tunalenga kuongeza kiwango cha uzalishaji, shabaha yetu iwe kuongeza tija ya uzalishaji wa karafuu katika kila

ekari. Kwa sasa uzalishaji wetu ni wastani wa **Tani 1.4** kwa ekari wakati nchi nyingine zinazalisha wastani wa **Tani 1.7 na Tani 1.8** kwa ekari. Hivyo, Serikali itaendelea kutafuta fursa za kutuongezea ujuzi na utaalam ili tuendelee kuongeza tija na ubora kwenye kilimo cha karafuu hapa nchini. Angalizo langu, *indhari* yangu, ni kwamba tunapotafuta njia za kisayansi kuongeza tija na uzalishaji tusishushe hadhi na ubora wa karafuu yetu.

**Ndugu Wananchi,**

Nimefarijika kusikia kwamba biashara ya magendo ya zao la karafuu inaendelea kupungua, ***hongereni sana*** Kamati za Ulinzi na Usalama kwa kusimamia hili. Hali hii imetokana na mikakati mizuri ya Serikali ikiwemo kutoa bei nzuri zaidi. Bei nzuri ikipatikana hapa watauza hapa nchini. Kwa hiyo nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuamua kutoa bei nzuri kwa wakulima wa karafuu.

Kwa upande wenu ZSTC hamna budi kuendelea kuwa karibu zaidi na wakulima kwa kuwapa nyenzo za kisasa, kutatua kero zao, kuwapa ushauri wa kitaalamu na kuwa na kanzidata inayoonesha ukubwa wa mashamba na makadirio ya mavuno.

Kwa sasa tunakadiria kwa kichwa. Tusikadirie kwa kichwa. Kama tulivyofanya kwa unyevu ambapo kwa sasa tunapima kwa mashine, na utabiri wa mavuno ya zao hili ufanyike kisayansi ili tuwe na uhakika wa tunachoenda kuvuna na kwa mipango yetu ya bajeti. Ni imani yangu kuwa tukiendelea kutumia njia hizi, pamoja na wakulima kuona mchango wao wa moja kwa moja kwa maendeleo ya nchi yetu, tutazidi kufanikiwa katika kudhibiti magendo ya zao la karafuu.

Kwa upande mwingine fikirieni uwezekano wa kufanya kilimo cha mkataba. Ninajua kuna mashamba mengi ya Serikali ambapo yalikuwa yapo tu. Mwaka juzi mlianza kuyatambua mashamba ya Serikali. Katika mashamba ya Serikali, ingieni mikataba na wakulima, wakulima wazalishe, wavune, muwape nyenzo alafu wakati wa mauzo mtajua nini cha kufanya. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila shamba linazalisha vile inavyotakiwa. Tukiyatupa kama tulivyoyatupa huko nyuma, watu wataingia, watavuna na watajimilika, na hatutakuwa na mpango maalum wa mashamba ya Serikali. Kwenye mashamba ya Serikali, ingieni mikataba na wakulima, toeni nyenzo wakulima wazalishe, ili tuvune vile tunavyotarajia.

## KUIFUNGUA PEMBA KIUCHUMI

**Ndugu wananchi,**

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina mipango mizuri ya kuifungua Pemba katika nyanja mbalimbali za maendeleo. SMZ inaendelea na mipango ya ujenzi wa miundobinu mbalimbali ikiwemo miradi ya bandari za kisasa Wete, Mkoani na Shumba Mjini. Mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Pemba nao unaendelea. Tunashuhudia ujenzi wa barabara mbalimbali ukiendelea. Haya yataongeza usafiri na usafirishaji wa watu na bidhaa kuingia na kutoka Pemba, na kwa maana hiyo itazidi kuvutia uwekezaji na kuleta fursa zaidi za ajira ndani ya kisiwa na Pemba.

Waziri nimelipokea lile ombi lako kuhusu ATCL (*Shirika la Ndege la Tanzania*). Nitaongea ili wajitahidi kuangalia kuwa na safari kuja Pemba. Lakini kwa sasa ATCL ni shirika la kibiashara. Kama safari zikikosa abiria wataacha tena kuja. Kukiwa na mizigo watakuja, wakikosa mizigo hawatakuja. Kwa sababu wanafanya biashara. Wanaelekea zaidi kwenye biashara. Hata Tanzania Bara hawaendi mikoa yote, wanakwenda mikoa ambapo kuna abiria na

kuna biashara. Ombi nitalipeleka lifikiriwe, lakini kuna masharti ya kibiashara inabidi pia yatazamwe.

Niipongeze pia SMZ; miezi miwili niliona unasainiwa mkataba wa kuendesha kiwanda cha kuchakata mwani Chamanangwe. Hizi ni hatua muhimu sana na nzuri katika kutekeleza uchumi wa bluu kwa Pemba. Mbali na mwani kuna mambo kadhaa kwenye uchumi wa buluu ambayo tunaweza kufanya Pemba. Nasi tunajitahidi kutafuta fedha kwa wahisani ambao wanaweza kutupa fedha ili tuingize vijana kwenye uchumi wa bluu.

Kwa upande wa Tanzania Bara tumeanza BBT – Jenga Kesho Iliyo Bora kwa vijana, na huku Zanzibar tumelileta pia kwenye sekta ya kilimo. Sasa tutatafuta fedha kuwaelekeza vijana kwenye uchumi wa buluu. Nilitembelea maonesho ya mazao ya uchumi wa bluu kule Unguja, na nikakuta kaa moja akifika kilo moja ndani ya Zanzibar anauzwa kati ya Shilingi 10,000 na 15,000. Lakini akitoka nje ya nchi, kaa moja wa kilo moja ni Shilingi 25,000. Hiyo ni kazi nzuri sana kwa vijana. Tuwawekee miundombinu, tuwape ujuzi, vijana waingie wafuge. Kuna soko la kutosha ulimwenguni

kwa mazao ya baharini. Uchumi wa buluu ndio utakaoleta ajira kwa vijana na niombe sana wakuu mliopo hapa tukajielekeze huko. Tujenge kesho bora ya vijana wetu kwa kuwaelekeza kwenye sekta za uzalishaji ambapo wanaweza kupata ajira na kujenga maisha yao.

Mbali na miundombinu ya kiuchumi, Serikali imeendelea pia kuwekeza kwenye huduma zinazoleta ustawi, ikiwemo huduma za afya. Hospitali tatu za Wilaya zimejengwa Kinyasini, Wilaya ya Wete, Micheweni, Wilaya ya Micheweni, na Vitongoji, hapa Wilaya ya Chakechake. Kabla ya hospitali hizi baadhi ya wananchi ilibidi wasafiri umbali mrefu kupata huduma za afya, ama iliwalazimu waende Hospitali ya Rufaa ya Mkoani, au Hospitali ya Mnazi Mmoja, Unguja, wengine Hospitali ya Taifa, Muhimbili. Leo, huduma zinazotolewa kote kule zinatolewa kwenye hospitali zetu za Wilaya. Haya ni maendeleo makubwa.

Wakati ule inapowalazimu ndugu wa wagonjwa kuwapeleka wagonjwa mbali, ilikuwa inachukua rasilimali fedha zao. Sasa fedha hizo zitatumika kwenye masuala mengine badala ya

kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi. Wagonjwa watapelekwa mbali pale itakapobidi lakini mambo mengi yatafanyika ndani ya nchi.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kuunga mkono utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu utakaoleta fursa zaidi za kiuchumi Pemba. Tutaunga mkono pia shughuli zote zinazolenga kuleta ustawi wa wananchi katika visiwa vya Unguja na Pemba.

**HITIMISHO**

**Ndugu wananchi**

Nikielekea kuhitimisha, nitumie fursa hii kuipongeza tena Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Rais Dkt Hussein Ali Mwinyi kwa kazi nzuri inayoifanya katika kukuza sekta ya kilimo kwa ujumla na hususan zao la karafuu. Uwepo wetu leo hapa ni kutokana na zao la karafuu.

Kwa upande wangu niahidi kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kutafuta masoko zaidi na kutoa msukumo zaidi kwenye zao hili.

Kwa upande wa ZSTC, hamna budi kuendelea kuwa karibu na wakulima wa karafuu. ZSTC ipo kwa ajili ya wakulima, inahudumia wakulima, na kazi yake ni kunufaisha wakulima wa karafuu, na si kujinufaisha yenyewe. ZSTC fanyeni ile kazi mliyoundiwa.

Nitoe wito pia kwa wakulima wa zao la karafuu kuongeza mikarafuu mipya na kuongeza uzalishaji, kuchuma karafuu zikiwa zimepea vizuri na kuanika kwa kutumia majamvi sambamba na kuuza karafuu ZSTC zikiwa safi.

Vilevile, ninawasihi wakulima wa zao la karafuu kuzingatia utaratibu wa Serikali wa kupokea malipo kwa njia za benki na mitandao ya simu. Hili ni jambo jema kwa kwa usalama wenu na fedha zenu.

***Baada ya maneno hayo, sasa nitamke rasmi kuwa, jengo la Uwekezaji la ZSTC (Karafuu Investment House) hapa Madungu limefunguliwa rasmi.***

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza**